# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

**MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.**

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mola anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa muhtasari huu na atupe usikivu na uelewa sote kwa pamoja.

Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa  mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunatoa pongezi maalum kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa nia yake ya dhati ya kuwaletea maendeleo endelevu wananchi wa Unguja na Pemba ambayo inadhihirika kupitia ufuatiliaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

Aidha, Kamati yangu inawapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kwa namna wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika uendeshaji wa nchi hii. Ni ukweli usiopingika kuwa, msaada wao una umuhimu mkubwa katika kuendeleza umoja na mshikamano wa wananchi na kufungua milango ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo inasimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara tano zifuatazo:

- Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji
- Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi
- Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda
- Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na
- Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara kwenye Wizara hizo na taasisi zinazozisimamia kwa Unguja, Pemba na Tanzania Bara kwa lengo la kufuatilia kwa kina utekelezaji wa shughuli za Wizara hizo na Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba sasa nichukue fursa hii kuwapongeza mawaziri wa Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati yetu akiwemo aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga, Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Mheshimiwa Shaaban Ali Othman, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Mheshimiwa Omar Said Shaaban, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale pamoja na timu zao za watalaamu kwa mashirikiano waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha kazi za Kamati. Kadhalika, napenda kuishukuru Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuipatia Kamati yetu miongozo iliyopelekea kufanya kazi zetu kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mara nyengine tena, napenda kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano makubwa waliyoyaonesha katika kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi wa hali ya juu. Naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii na makatibu wao mmoja baada ya mwengine kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Mohammed Ali Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
9. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu
10. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
11. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
12. Ndg. Azmina Khamis Hamad - Msaidizi

## OFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji imeundwa kwa Idara saba, Taasisi mbili zinazojitegemea pamoja na Bodi zake na Ofisi Kuu Pemba na ina jumla ya Wafanyakazi 395 ( kati ya hao 311 wako Unguja na 84 wako Pemba) inayojumuisha Wanawake 205 na Wanaume 190.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilmo inaipongeza Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kuvuka lengo la makusanyo ya mapato kwa mwaka 2023/2024 ambapo hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2023, Afisi imefanikiwa kukusanya jumla ya TSh. 2,434,247,764 sawa na asilimia 167% ya lengo lilopangwa, kupitia vianzio vyake 4, ikiwemo ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa matumizi, hadi kufikia Disemba 2023, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu A07 ilipatiwa jumla ya Tsh. 2,964,835,808 sawa na asilimia 77 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TSh. 2,138,068,789 za mishahara sawa na asilimia 100 ya makadirio na TSh. 826,767,019 sawa na asilimia 49 ya makadirio kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na hakuna fedha zilizoingizwa kwa miradi ya Maendeleo.

Aidha, kupitia fungu A08, Afisi ilipatiwa jumla ya Tsh. 6,264,675,608 sawa na asilimia 75.7 ya utekelezaji wa Programu zote kwa kipindi hicho. Kati ya hizo Tsh. 2,171,999,368 zilitumika kwa Mishahara ambayo sawa na asilimia 102.9 ya makadirio. Aidha, Tsh. 246,850,000 ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo sawa na asilimia 43.5 ya makadirio. Na Tsh.3,845,826,240.00 sawa na asilimia 68.7 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**PROGRAMU KUU YA KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI**

**Mheshimiwa Spika,**

Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni jambo ambalo linahitaji uzalendo na kujitoa kwa hali na mali katika katika kuwapa fursa za mikopo makundi mbalimbali ya wajasiariamali, vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili waweze kujikwamua kuichumi kwa kujikusanya pamoja na kuanza kufanya shughuli za uzalishaji mali zitakazoweza kuwapatia kipato ambacho

kitakweza kuendeleza maisha yao. Kwa kutambua umuhimu wa shughuli za uwezeshaji kwa jamii, Serikali ilianzisha Wakala wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi (Zanzibar Economic Empowerment Agency) kwa Sheria namba 2 ya mwaka 2022. Kamati inaunga mkono juhudi hizo za Serikali katika uwezeshaji wa wananchi kiuchumi

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na kitendo cha Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kutekeleza takwa la kisheria la kuipatia Wakala wa Uwezeshaji kiuchumi asilimia 10 ya mapato ya ndani yanayokusanywa na Mamlaka hizo. Hali inayopelekea maombi mengi kutoka kwa makundi hayo kukosa mikopo kutokana na uhaba wa fedha. Hivyo, Kamati inaiagiza Wizara kuwasiliana na Wizara inayosimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hayo, suala la kuwapatia elimu wananchi juu ya njia bora za uanzishaji wa miradi yenye tija na inayoweza kukopesheka kupitia mifuko mbalimbali ya uwezeshaji ni jambo muhimu la kulitilia mkazo kwa upande wa Wakala, kwa vile yapo maombi mengi ya mikopo yameshidwa kuzingatiwa kutokana na miradi inayoombewa kukosa sifa ya kupatiwa mikopo na hatimae kuwepo kwa malalamiko kwa wananchi ya kukosa mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kuruhusu uwekezaji katika visiwa vidogo vidogo kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na kuweza kuingizia Serikali jumla ya Dola za Kimarekani Milioni ishirini na sita (USD 26,000,000) kama ni mahari na Dola za Kimarekani Milioni mia tatu themanini na nne nukta nne (USD 384.4 milioni) zinatarajiwa kuekezwa katika visiwa 15 ambavyo tayari vimeshapata Wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Hii ni hatua kubwa ya kupigiwa mfano katika suala la kuendeleza uwekezaji nchini ambao utaongeza fedha za kigeni na kuinua kwa kasi uchumi wa

Zanzibar. Hata hivyo, Kamati inaagiza uwekezaji huo uende sambamba na upatikanaji wa fursa za ajira kwa wazawa kwa lengo la kuinua hali za maisha ya watu Zanzibar kiuchumi. Aidha, suala la uhifadhi wa mazingira lizingatiwe kikamilifu katika visiwa hivyo ili kuendelea kubaki na haiba yake.

**PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE.**

**Mheshimiwa Spika,**

Utaratibu wa fedha za matumizi ya kawaida (OC) kutoingia kwa wakati na kwa kiwango sahihi kwa mujibu wa 'Cash flow' unakwamisha jitihada za Wizara/Idara na Tasisi za Serikali katika kutekeleza shughuli zake ipasavyo.

Hali hii imedhihirika kupitia ziara ya Kamati katika Wizara na Taasisi tofauti . Kwa mfano, Idara ya Afya na Usalama Kazini haina ufanisi katika kufanya kazi zake za ukaguzi wa sehemu za kazi kutokana na kukosa vitendea kazi vya kisasa vya ukaguzi kunakosababishwa na uhaba wa fedha za matumizi mengineyo, na badala yake hushirikiana na Taasisi ya OSHA kutoka Tanzania Bara katika kufanya ukaguzi jambo ambalo huikosesha Serikali mapato.

**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Idara sita na taasisi nne zinazojitegemea. Idara hizo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Ukijumuisha Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi), Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Idara ya Hifadhi za Baharini na Afisi ya Afisa Mdhamini – Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imekadiriwa kukusanya Mapato ya jumla ya **Shilingi 5,727,275,209** kutoka

vianzio vyake 4 vya Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Wizara ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 3,217,333,115** na imekusanya jumla ya **Shilingi 2,673,673,702** sawa na asilimia **83.1** ya makadirio. Kamati inaiagiza Wizara kuongeza juhudi kwenye ukusanyaji wa mapato ili kuchangia kwenye pato la Taifa.

Kwa upande wa matumizi, Kwa kipindi cha Mwezi wa Julai hadi Disemba, 2023 Wizara imepata jumla ya **Shilingi 4,178,486,074.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,813,411,869** ni kwa kazi za kawaida, ambapo **Shilingi 2,121,556,507** ni Mishahara, **Shilingi 341,144,048** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, na **Shilingi 1,350,711,314** ni Ruzuku kutoka SMZ (ambapo **Shilingi 67,748,000** kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar, **Shilingi 1,083,129,688** kwa Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na **Shilingi 199,833,626** kwa Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO).

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Pogramu hii inalenga kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini na inajumuisha ndani yake programu ndogo mbili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanikiwa kuwa na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za baharini Zanzibar (ZAFIRI) ambayo imepitishwa na Baraza lako tukufu kwenye mkutano wa 13 wa Baraza uliofanyika Disemba 2023. Ni imani yetu kuwa, Taasisi hii itafanya kazi zake kwa ufanisi zaidi na kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar imelenga kuboresha maisha ya wananchi kupitia sera ya Uchumi wa buluu na uvuvi. Katika kufanikisha lengo hilo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kushirikiana na Taasisi ya Marine and Coastal Community Conservation (MCCC) imejenga kituo cha kutotolesha na uleaji wa vifaranga vya matango bahari katika kijiji cha Kibaridi Pujini Pemba pamoja na kituo cha uzalishaji wa samaki na matango bahari

Beital Ras kwa upande wa Unguja. Vituo hivi vilijengwa kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa vifaranga vyenye ubora kwa ajili ya ufugaji endelevu wa samaki na matango bahari.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha vituo hivi na inaitaka Wizara kuviendeleza kwa kuvipatia nyenzo na utaalamu ili viweze kufikia lengo lililokusudiwa la kupunguza uvunaji wa matango bahari kutoka baharini na kukuza uchumi wetu. Mara baada ya kusimama imara vituo hivi, tunashauri kuanzishwa kwa vituo vyengine ili kuendeleza uzalishaji wa mazao ya baharini nje ya bahari ambao ndio unaochangia kwenye pato la nchi kadhaa za ukanda wa pwani na visiwa kama yetu.

Kutokana na azma hii nzuri, Kamati inaishauri jamii ya Wazanzibari kushiriki katika shughuli mbali mbali za maendeleo ikiwemo matumizi endelevu ya rasilimali za bahari kama vile ufugaji wa samaki na matango bahari ili kuongeza kipato chao na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kutambua fursa iliyopo kwenye biashara ya dagaa, Serikali kupitia Kampuni ya Uvuvi ZAFICO imeamua kuirasimisha na kuiongezea thamani ili ilete tija kubwa kwa wafanya biashara wenyewe na Taifa kwa ujumla ambapo miradi miwili imeanzishwa kwa ajili ya kusarifu na kuongeza thamani ya dagaa. Miradi hiyo ni Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa - Ndagoni na Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa - Kama. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia fursa iliyopo nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imesikitishwa na kutokamilika kwa wakati ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa kilichopo Kama, ambapo ilitarajiwa kwa lot namba 1 Mradi huo iwe imekamilika kwa asilimia 100 ifikapo Disemba 2023. Wakati Kamati ilipotembelea Mradi huo tarehe 19/01/2024, ujenzi wa Lot 1 umefikia asilimia 70 ambapo sehemu iliyobaki ni ujenzi wa land scape ambao imechelewa kutokana na sababu mbalimbali zilzoelezwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiagiza Wizara kupitia Kampuni ya ZAFICO kusimamia vizuri ujenzi wa Mradi wa Kiwanda cha kusarifu dagaa - Kama kwa (phase) zote mbili ili kuweza

kukamilika kwa wakati na tija iweze kupatika kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ilitembelea baadhi ya Kampuni za utengezaji wa boti ambazo Serikali imeingia mikataba nazo na kubaini kasi ndogo ya ujenzi wa boti kutokana na sababu tofauti. Pia, Kamati imebaini kuwa baadhi ya kampuni zilizopewa kazi hazikuwa na uwezo wala sifa ya kufanya kazi hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiagiza Wizara kuwasimamia ipasavyo wakandarasi wote ambao wamewapa kazi ya kutengeneza Boti na kuhakikisha wanazikamilisha kazi zao kwa wakati kwa lengo la kuwapatia wavuvi Boti zao.

Aidha, Kamati inaagiza uongozi wa Wizara kwa kushirikiana na Uongozi wa CRDB kuharakisha mchakato wa kupatiwa bot wananchi au vikundi ambavyo vimekaguliwa na kuonekana vina sifa ya kupatiwa mkopo huo.

## WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inaundwa na Idara na Taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi katika kuwaletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Idara hizo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula, Idara ya Umwagiliaji Maji, Idara ya Misitu, Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Afisi ya Afsa Mdhamini –Pemba.

Taasisi zinazojitegemea ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Matrekta na Zana za Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 Wizara ilikadiriwa kupata jumla ya TZS bilioni 21.211 (TZS bilioni 16.886 ni mishahara, TZS bilioni 4.324 ni matumizi ya kawaida na TZS bilioni 8.300 ni ruzuku). Kwa upande wa fedha za Maendeleo Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 68.524 (TZS bilioni 25.000 ni kutoka SMZ na TZS bilioni 45.524 ni kutoka kwa Washirika wa

maendeleo.

Kwa upande wa matumizi, Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 Wizara imepata jumla ya TZS bilioni 28.801 (TZS bilioni 12.680 mishahara, TZS bilioni 1.234 ni kwa matumizi ya kawaida na TZS bilioni 14.886 ni kwa miradi ya maendeleo kutoka kwa Washirika wa maendeleo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilifanya ziara katika miradi mbali mbali ya umwagiliaji kwa lengo la kutathmini maendeleo yake pamoja na tija iliyopatikana, kutokana na ukweli kwamba fedha nyingi zimeelekezwa kwenye kilimo cha umwagiliaji ikiwa ni utekelezaji wa mpako wa Taifa wa uhakika wa chakula. Kati ya Miradi iliyotembelewa na Kamati ni Miradi ya Umwagiliaji maji katika Bonde la Kinyasini (Unguja). Kupitia ziara hizo, Kamati ilishuhudia miundombinu isiyoridhisha, upungufu wa vitendea kazi, kukosekana kwa teknolojia pamoja na uhaba wa rasilimali watu.

Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiagiza Wizara kusimamia kwa makini miradi hii na kurekebisha miundombinu na kupeleka watendaji na zana za kutosha ili kufikia lengo la Serikali la uhakika wa chakula nchini.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kupitia Idara ya Kilimo, kuwashirikisha kikamilifu wananchi wanaoishi karibu na maeneo yanayotarajiwa kuanzishwa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kupatiwa ushauri kwani baadhi ya wakulima wa maeneo hayo wana uzoefu wa kutosha juu ya masuala ya kilimo cha umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Uzalishaji wa mpunga ni shughuli inayoendelea kusimamiwa na Wizara hii, ingawa inakabiliwa na changamoto nyingi zinazokwaza juhudi za wakulima. Kamati imebaini kuwa baadhi ya matrekta hushindwa kuingia kabisa katika mabonde ambayo yamewekewa miundombinu mipya ya umwagiliaji kutokana

na miundombinu hiyo kutozingatia aina ya matrekata tuliyonayo hali inayopelekea wakulima kukosa huduma stahiki na Wakala kukosa mapato. Hivyo, Kamati inaiagiza Wizara kurekebisha miundombinu ya umwagiliaji ili iendane na matrekta yaliyopo nchini kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakulima kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Ili huduma za matretka ziweze kuimarika ni vyema Wakala kuongeza idadi ya matrekta mapya kwa vile idadi iliyopo sasahivi haitoshi kuhudumia wananchi wote kwa wakati mmoja jambo ambalo linakwamisha juhudi za wakulima wetu katika kilimo cha mpunga. Pia, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kuyafanyia matengenezo matrekta 14 ambayo yameharibika ili kuanza kufanya kazi na kupunguza changamoto ya uhaba wa matrekta ambayo Wakala wa huduma za matrekta na zana za kilimo unakabiliana nayo kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo inaipongeza Serikali kwa kuanzisha mradi wa Ujenzi wa maghala ya kuhifadhia chakula ambao ulilenga kuondosha kabisa madhara ya Sumu Kuvu nchini, ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kutekeleza miradi ya ujenzi wa maghala 14 kwa Tanzania nzima, kati ya hayo maghala mawili kujengwa Zanzibar, moja kwa upande wa Pemba na moja kwa upande wa Unguja.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa ghala la chakula la Dodeani, Kamati imesikitishwa kuona Mradi huu bado haujafikia lengo lililokusudiwa. Kutokana na hali hii, Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo ya Zanzibar na Tanzania Bara na kukubaliana mambo mbalimbali likiwemo la kuusimaisha mradi huo na mkandarasi kuchukuliwa hatua za kisheria.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha vituo vya mifugo katika maeneo tofauti kwa lengo la kupokea wanyama wote wanaotoka Tanzania Bara, kuwapima pamoja na kuwaweka karantini kabla hawajaingia mitaani kwa shughuli nyengine za kibinaadamu. Kimsingi, vituo hivi vinasaidia sana kudhibiti uingizaji holela wa wanyama na kuepusha uingizaji wa maradhi kwa wanyama.

**Mheshimiwa Spika,**

Vituo hivi vinakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo ufinyu wa ofisi, Uhaba wa vitendea kazi. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiagiza Wizara ya Kilimo kufanya utaratibu wa kuvijengea Ofisi vituo hivyo zenye uwezo wa kuhudumu wateja wanaofika kupatiwa huduma ili watendaji wanaofanya shughuli zao vituoni waweze kuratibu shughuli zao kwa ufanisi.

Aidha, Kamati inashauri wananchi wapewe elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa miradi ambayo Serikali inawekeza kwa ajili yao. Kwa kufanya hivyo ndio tutaweza kupata uhakika wa ulinzi kwa miradi yote nchini na itawasababisha kuilinda na kuienzi miradi hiyo.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini changamoto ya uharibifu wa Misitu unaoendelea kufanywa na wananchi wanaoishi karibu na misitu yetu ya hifadhi kwa matumizi mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na kukata kuni, kupasua mbao na kupiga tanu za mkaa, hali inayopelekea upotevu wa miti mikubwa ya asili iliyomo ndani yake. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu, kuendelea kushirikiana kikamilifu na viongozi wa shehia zilizozunguka eneo la misitu juu ya suala zima la kutekeleza majukumu katika kuilinda na kuhifadhi pamoja na kununua vifaa vyote vya ulinzi vinavyohitajika ili waweze kupambana na waharibifu wa rasilimali hiyo.

WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote. Idara hizo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Sera na Utafiti, Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko, Idara ya Maendeleo ya Viwanda, Afisi ya Afsa Mdhamini Pemba.

Kwa upande wa Taasisi na Mashirika ya Wizara ni haya yafuatayo: Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), Wakala wa Usasjili wa Biashara na Mali, Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC), Taasisi ya Viwango zanzibar (ZBS), Mamlaka ya Usimamizi wa leseni, Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo, vidogo na vya Kati (SMIDA), Tume ya Ushindani Halali wa Biashara, Baraza la Ushindani wa Biashara na Wakala wa Vipimo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Biasharana Maendeleo ya Viwanda imepanga kutekeleza vipaumbele katika maeneo makuu matatu (3) ambayo ni kuendeleza Ujenzi kwenye eneo la Maonesho ya kibiashara Dimani; Kuratibu ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (Convention Centre); Kujenga Vituo Jumuishi kwa ajili ya Urasimishaji Biashara, na kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda ya Dunga na Chamanangwe. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweka vipaumbele vinavyostahiki kwa maendeleo ya wajasiriamali na sekta ya biashara nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs. bilioni 1.750 kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa huduma zinazotolewa. Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya Tzs. milioni 490.69 zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo ni sawa na asilimia 61 ya makadirio yamakusanyo. Aidha, Baraza la Udhibiti Mfumo wa Utoaji Leseni (BLRC) lilipanga kukusanya jumla ya Tzs. milioni 32.97 kutoka katika Mamlaka za Serikali Zinazotoa leseni, hadi

kufikia Disemba 2023, Baraza limekusanya Tzs. milioni 42.02 kutoka katika mamlaka hizo ambazo zimeingizwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Biasharana Maendeleo ya Viwanda ilipangiwa kutumia jumla ya Tzs. bilioni 35.952 kwaajili ya kutekeleza programu zake kuu tatu (3). hadikufikia Disemba2023, jumla ya Tzs. bilioni 10.930 zimetumikasawa na asilimia 64 kwa ajili ya matumizi hayozilitumika.

**Mheshimiwa Spika,**

Sekta ya biashara ndio uti wa mgongo wa Wizara hii ambapo zao la karafuu ndio zao kuu la biashara nchini. Kamati ilifanya ziara katika vituo mbalimbali vya ununuzi wa karafuu na kujionea shughuli za ununuzi zikiendelea hiku zikikabiliwa na changamoto kadhaa. Kwa mfano, katika kituo cha ununuzi wa karafuu Wete Wakulima wengi hawana taaluma nzuri juu ya utaratibu wa kupunguza unyevu katika karafuu ambazo wanazozifikisha kituoni hapoo, jambo ambalo linasababisha malalamiko mengi kutoka kwa wakulima pale wanapotajiwa grade au kiwango cha karafuu zao.

Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Wizara kukaa na wakulima wa karafuu ambao ndio wadau wao wakuu kwa lengo la kuwapa elimu juu ya masuala mbali mbali yanayohusiana na zoezi zima la ununuzi ikiwemo matumizi ya machine ya kuchekechea, mizani za kupimia na hata umuhimu wa kuwepo kwa kifaa cha kupimia unyevu wa karafuu pindi zikifika kituano hapo. Hii itajenga ukaribu na kuaminiana baina wa watendaji wa kituo na wakulima na kupelekea mwendelezo mzuri wa zao letu hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile suala la biashara ya karafuu lina ushindani mkubwa duniani, Kamati inaiagiza Wizara kupitia Shirika la ZSTC kujitangaza zaidi kimataifa pamoja na kutumia vyombo vyetu vya ndani kwani biashara ni matangazo. Ingawa brand yetu inajulikana duniani kote lakini kwa kuendelea kujitangaza itapekekea kujifungua kibiashara hasa ukizingatia zipo nchi za visiwa ambazo pia

zinazalisha karafuu na kuuza katika soko la dunia.

**Mheshimiwa Spika**

Kamati imeridhika kuona hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa kiwanda cha mwani pamoja na viwango vya miundombinu ya kiwanda hicho ingawa kuna mapungufu madogo madogo ambayo tuliyabaini na kuyatolea muongozo kwa ajili ya kuboresha kiwanda chetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na pongezi juu ya ujenzi wa kiwanda hiki ila kuna ucheleweshaji wa kutiliana saini kwa makubaliano baina ya Serikakli ya mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya Uingereza juu ya suala zima la uendeshaji wa kiwanda hicho ambayo ni changamoto iliyobainika kupitia ziara ya Kamati, kwani hadi sasa ni mzunguko wa pili kamati inatembelea eneo hilo na kubaini bado mkataba huo wa makubaliano ya uendeshaji haujaekwa saini tofauti na matarajio yetu.

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kumaliza mchakato wa mpango wa ununuzi wa mashine na utiaji saini wa uendeshaji wa kiwanda hiki ili kianze uzalishaji kwa maslahi ya wakulima wa mwani na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kutafuta mwekezaji ili Nyumba iliyopo Sinza ivunjwe na kuanzishwa mradi mkubwa kama vile ujenzi wa Gorofa lenye nyumba za kukodisha au ujenzi wa parking za kisasa ambazo gari zinakaa gorofani ili Shirika liweze kufaidika. Pia, Kamati inashauri  Duka la Shirika lililopo Dar-es-salaam liuze bidhaa zinazoendana na Shirika letu na kuachana na kuuza bidhaa nyengine ndogo ndogo zisizozalishwa na shirika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kwamba Taasisi yetu ya ZBS sio mwanachama wa Jumuiya ya  Taasisi za Viwango za Afrika mashariki pamoja na ile ya Afrika kwa ujumla.Kwa mnasaba huo, ZBS wanashiriki vikao vya Nchi wanachama kama waangalizi tu kitu ambacho kama Serikali hakitopata tija kubwa kwani hatutokua na uwezo wa kufanya maamuzi yoyote pindi yakipitishwa ndani ya

vikao hivyo.

Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Viwanda kuharakisha mchakato wa kuendelea kuboresha maabara za ZBS ili ziweze kuwa na viwango vinavyokubalika kwa lengo la kuiwezesha Taasisi yetu hii kua mwanachama kamili katika jumuiya za Taasisi za viwango za Afrika mashariki pamoja na ile ya Afrika kama ilivyo Taasisi ya viwango (TBS) iliopo Tanzania bara.

**Mheshimiwa Spika**,

Changamoto nyengine iliyojitokeza ni ile ya ucheleweshaji wa kuanza kazi mradi wetu wa ukaguzi wa vyombo vya moto. Hii imetokana na kukwama kwa kontena za vifaa za taasisi kwa kukosa msamaha wa kodi, kontena ambazo ndani yake kuna mashine zinazotarajiwa kutumika katika shughuli za mradi huu. Kuendelea kukwama bandarini kwa kontena zile kutapelekea kudhorotesha maendeleo ya Taasisi hii na Serikali kwa ujumla.Hivyo Tunaiomba Wizara ya Fedha ikae na Taasisis yetu hii ya ZBS ili waweze kutafuta mbinu za kulitatua tatizo la mkwamo wa vifaa ambavyo uwepo wake vitasaidia Serikali kuengeza mapato nchini.

## WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ina dhamana ya kusimamia Sekta Kuu mbili ambazo ni Utalii na Mambo ya Kale. Sekta hizi hujumuisha Kamisheni moja, Idara nne, Mamlaka moja na Ofisi Kuu Pemba ambazo ni: - KamisheniyaUtalii Zanzibar, IdarayaUtalii, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na OfisiKuu Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa “Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria”. Kwa sasa Wizara ipo katika hatua za utekelezaji wa mradi huo ambao ulianzwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha2022/2023. Katika

mradi huu, maeneo yanayofanyiwa matengenezo ni pamoja na eneo la kihistoria la Mangapwani Unguja na eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba, eneo la kihistoria la Maruhubi na kuimarisha Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni – Unguja. Hata hivyo, Kamati imeiagiza Wizara kuondoa changamoto zilizojitokeza kwenye mradi huo ili kufikia malengo tuliojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa kuwa na mashirikiano makubwa na Bodi ya Utalii Tanzania ambayo ndiyo chombo kinachotoa miongozo kwenye sekta ya utalii nchini. Mashirikiano hayo yanaiweka Kamisheni kuwa karibu na soko la utalii duniani na kuendelea kupata njia zaidi za kufanya promotion ya utalii wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na juhudi kubwa zinazooneshwa na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii, Kamati imebaini kuwa Kamisheni inakwazwa na changamoto kadhaa ikiwemo Ukosefu wa ofisi kwa watendaji wa Kamisheni ya Utalii: Jengo linalotumika ni la kukodi na halina nasafi za kutosha kwa maafisa wote, hivyo maafisa hulazimika kukaa katika sehemu zisizo rasmi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali Kamati inashauri Serikali kuipatia Kamisheni jengo la kisasa linalolingana na uzito wa kazi zake.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba muhtasari huu usomwe pamoja na Ripoti ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo tayari imo kwenye vishkwambi vyetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni matumaini ya Kamati kuwa maoni, ushauri na maagizo yaliyotolewa kwa Taasisi hizo yatasaidia katika kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, kuongeza uwajibikaji kwa viongozi na wanaoongozwa, kuongeza pato la Taifa na


kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

Mwisho, Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Uongozi wa Baraza la wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa ulioiwezesha kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kuandaa ripoti kama inavyostahili.
Napenda kuwashukuru tena Wajumbe wako kwa utulivu wao wa kuniskiliza wakati wa kuwasilisha muhtasari huu wa ripoti ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kutoa hoja.

Ahsante,



Mhe. Mtumwa Peya Yussuf,

Mwenyekiti,

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**